



Press release

Dar es Salaam Msafara wa Baisikeli 2010

Wiki ya Umoja wa Ulaya

“Usafiri kwa Wote”



Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam tunaandaa Msafara wa Baisikeli Dar es Salaam 2010 ndani ya Wiki ya Umoja wa Ulaya, utakaotokea Jumapili tarehe 9 mwezi wa tano 2010 kuanzia saa mbili asubuhi uwanja wa Mnazi Mmoja. Huu utakuwa ni msafara wa baisikeli wa tano Dar es Salaam; msafara hufanyika kila mwaka tangu mwaka 2006.

Kwenye Msafara wa Baisikeli, idadi kubwa ya wapanda baisikeli huendesha baisikeli pamoja kwenye maeneo ya jiji. Tunaendesha taratibu - siyo mashindano wala mbio. Wapanda baisikeli wote wa Dar es Salaam wanakaribishwa – vijana na wazee, wanaume na wanawake, na walemavu, na baisikeli za aina zote zinakaribishwa – baisikeli za kawaida, maguta, baisikeli za mikono za walemavu. Msafara utaanzia Uwanja wa Mnazi Mmoja, utafuata Barabara ya Bibi Titi Mohammed, Barabara ya Kawawa, Kariakoo na utarudi tena Mnazi Mmoja.

Tunashukuru sana wadhamini wa msafara wa baisikeli, Umoja wa Ulaya Tanzania, na tunafurahi kufanya msafara ndani ya Wiki ya Umoja wa Ulaya. Baadhi za nchi za Umoja wa Ulaya, mfano Netherlands na Denmark, wana miji na majiji mazuri sana kwa wapanda baisikeli na wanahamasisha baisikeli kama chombo cha usafiri ambacho ni kizuri kwa mazingira, kizuri kwa afya, kinapunguza msongamano wa magari na kinaweza kutumiwa na watu wote.

Zawadi za baisikeli tano, baisikeli za walemavu tatu, helmeti 20 na reflecta jaketi 200 zitasambaza kwa washiriki.

Kauli mbiu ya msafara wa baisikeli wa mwaka huu ni “Usafiri kwa Wote”. Baisikeli ni chombo kinachoweza usafiri wa haraka, mlango hadi mlango, usafiri wa bei nafuu, kwa jamii yote – matajiri na masikini, walemavu, wazima, vijana na watoto. Wapanda baisikeli wote (wa kawaida na walemavu) wanahitaji mazingira mazuri na salama barabarani, na barabara zinazoweka kipau mbele usafiri usiyo wa moto. Kwa hiyo, UWABA tunaomba kila barabara kubwa iwe na njia maalum za wapanda baisikeli (kama Barabara ya Nyerere), magari yositumie service roads kugesha, kutanua foleni wala kuendesha kwa haraka, na sheria za kuepuka uendeshaji wa hatari na mwendo wa kasi zitekelezwe vizuri, na barabara ndogo ziwe na matuta kuzuia magari kwenda kwa kasi. UWABA tunaomba vyama vya siasa kuweka masuala muhimu haya kwenye ilani za uchaguzi za mwaka 2010.

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)

UWABA ni NGO iliyoanzishwa Januari 2006 na wapanda baisikeli wa Dar es Salaam. Kwa sasa ina wanachama zaidi ya 200, wote wanatumia baisikeli kama chombo cha usafiri cha kila siku hapa Dar es Salaam. Malengo ya UWABA ni kuhamasisha baisikeli kama chombo kizuri cha usafiri Dar es Salaam, kuhamasisha serikali kuboresha usalama na mazingira kwa wapanda baisikeli, kulinda haki za wapanda baisikeli, kuhamasisha waendesha magari kuheshimu wapanda baisikeli na kuelimisha wapanda baisikeli kuhusu usalama barabarani. UWABA tunakutana kila jumamosi saa nne asubuhi kwenye ofisi yetu Manzese Sisi kwa Sisi. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye tovuti yetu www.uwaba.or.tz au kwa simu - mwenyekiti Mejah Mbuya (0713652642) au katibu Elaine Baker-Guni (0715568512).